



Our Ref: MK/GEN/05/013/110

Date: 20/05/2021

**TAMKO LA BAKWATA JUU YA VITENDO VYA KINYAMA NA
UADUI VYA ISRAIL KATIKA ARDHI YA TAIFA LA PALESTINA**

Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) linatoa tamko kulaani vitendo vya kinyama na uadui dhidi ya Taifa la Palestina na kuuwa raia wasio na hatia.


Vitendo hivi vinakwenda kinyume na misingi na haki za kibinadamu. Pia vinapingana na misingi ya dini kuu Duniani ikiwemo dini yetu ya Kiislamu.

Kwa tamko hili BAKWATA linaitaka Jumuiya ya Kimataifa, kuchukua hatua husika kusitisha udhalimu huu usio kubalika.

Aidha BAKWATA inawataka Waislamu wote Tanzania kuitumia Swala ya Ijumaa kusoma dua maalum kuliombea Taifa la Palestina na kuendelea na dua za Kunuti katika Swala zote tano kumuomba Mungu alinusuru Taifa la Palestina na Ulimwengu kwa jumla dhidi ya balaa hili kubwa na mabalaa mengine yote Ulimwenguni.

Mwenyezi Mungu tunakuomba uufanye Ulimwengu uione batili katika vazi lake la batili na uwaruzuku kuiepuka na utuoneshe haki katika vazi lake la haki na uturuzuku kuifuata na kuitetea.

Aamin ya Rabbal alaamiin.


Sheikh Abubakar Zubeir bin Ally
SHEIKH MKUU NA MUFTI WA TANZANIA

